**MAELEZO KUHUSU UANDAAJI WA MWONGOZO WA UREKEBU WA SHERIA (*LAWS REVISION MANUAL*)**

Onorius J. Njole, Mwandishi Mkuu wa Sheria;

Mheshimiwa Jaji Prof. Ubena J. Agatho, Jaji wa Mahakama Kuu Divisheni ya Biashara;

Bi. Sarah Barahomoka, Mwandishi Mkuu wa Sheria mstaafu na Mwenyekiti wa Kikosi Kazi;

Esther Manyesha, Mwandishi wa Sheria Mkuu mstaafu, Sehemu ya Urekebu;

Richard Mbaruku, Mwandishi wa Sheria Mkuu mstaafu Sehemu ya Urekebu wa Sheria;

Afacky Msigala, Mrekebu wa Sheria mstaafu; na

Ally Machupa, Mpiga Chapa mstaafu;

Awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kutujalia uhai na afya njema na kwa kutuwezesha sote kuwepo hapa kushiriki katika kikao kazi hiki. Pia, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kusimama mbele ya kikao hiki kutoa maelezo juu ya uandaaji wa mwongozo wa urekebu wa sheria.

**Ndugu wajumbe;**

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kupitia Ofisi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria pamoja na kuwa na majukumu ya uandishi wa sheria, pia, ina jukumu la urekebu wa sheria zote za nchi. Jukumu hili linatekelezwa na Sehemu ya Urekebu. Aidha, urekebu wa sheria unasimamiwa na Sheria ya Urekebu wa Sheria, Sura ya 4. Sheria hii imebainisha masuala ambayo

yatafanyika wakati wa zoezi la urekebu kuanzia kutolewa kwa Tamko la Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Urekebu wenyewe, tamko la kuanza kutumika kwa sheria na toleo la urekebu, utunzaji wa nakala za sheria za urekebu hadi usambazaji pamoja na urekebu wa nyongeza, yaani, *Annual Supplement*.

**Ndugu wajumbe;**

Kwa muda mrefu, Ofisi imekuwa ikitekeleza urekebu wa sheria mahsusi baada ya kupokea maombi kutoka katika taasisi au Wizara zinazosimamia sheria husika. Hata hivyo, katika kukabiliana na changamoto ya Sheria kushindwa kusomeka kwa urahisi kutokana na kuwa na marekebisho mengi, Mwaka 2019, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ilianza zoezi la urekebu wa Sheria Kuu 446 ili kutoa Toleo la Sheria zilizofanyiwa Urekebu la Mwaka 2023. Ofisi imekamilisha urekebu wa sheria hizo 446 na Toleo hilo la urekebu linatarajiwa kuzinduliwa mwezi Novemba mwaka 2024.

**Ndugu wajumbe;**

Mwongozo unaoandaliwa unakusudia kutatua changamoto ambazo Ofisi imekuwa ikikutana nazo wakati wa utekelezaji wa mazoezi ya Urekebu wa Sheria. Hivyo, mwongozo mnaoenda kuuandaa unatarajiwa kubainisha mahitaji ya kisheria wakati wa urekebu wa sheria, aina za urekebu, hatua kuu za urekebu na masuala ya msingi ya kuzingatiwa wakati wa utekelezaji wa zoezi la urekebu. Aidha, Mwongozo huo utatakiwa kuweka viwango vya utendaji vinavyopaswa kuzingatiwa katika kila hatua ya urekebu, usimamizi na utunzaji wa nyaraka, misingi ya urekebu pamoja na ushirikishwaji wa

wadau. Hivyo, ni imani yangu kuwa mwongozo utakaoandaliwa utarahisisha zoezi la urekebu wa sheria na hivyo kupunguza gharama za uandaaji wa matoleo ya urekebu yajayo, kudumisha muundo na mtindo wa uandishi wa sheria za nchi pamoja na kuimarisha utunzaji wa nyaraka.

**Ndugu wajumbe;**

Kwa kuzingatia umuhimu huu, ninawaomba wajumbe wote kutekeleza jukumu hili kwa weledi ili kufikia lengo la kupata mwongozo bora utakaotumiwa na maofisa wetu katika kutekeleza jukumu la urekebu wa sheria. Ni imani yangu kuwa matokeo ya kazi hii yatakuwa msingi imara utakaoendelea kusaidia mazoezi ya urekebu yanayofuata.

**Ndugu Wajumbe;**

Kazi hii inashirikisha wajumbe wabobevu ambao ni wanasheria wenzetu waliowahi na wanaoendelea kulitumikia Taifa letu wakiwemo Bi. Sarah Barahomoka ambaye aliwahi kushika nafasi ya Mwandishi Mkuu wa Sheria, Bi. Esther Manyesha na Bw. Richard Mbaruku waliowahi kuwa Waandishi wa Sheria Wakuu Wasaidizi, Bw. Afacky Msigala aliyekuwa Afisa Urekebu Mwandamizi na Ally Machupa, Mpiga Chapa mstaafu kutoka Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali. Nimetaarifiwa kuwa katika Timu hii watakuwepo pia wataalam kutoka Ofisi ya Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali wakiongozwa na Mpiga Chapa Mkuu wa Serikali mwenyewe. Ni imani yangu kuwa mchanganyiko huu wa Timu utakuwa na tija kubwa katika utekelezaji wa jukumu hili.

Aidha, nawashukuru kwa dhati kwa kukubali kutumia muda wenu kwa ajili ya kutusaidia katika kazi hii. Ninafahamu baadhi yenu mmekuwa

mkishirikiana nasi katika kazi mbalimbali kama vile kuandaa miongozo, mafunzo n.k. Ushiriki wenu katika kazi hizi umekuwa na mchango mkubwa katika kuboresha utendaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Ofisi yetu bado inaendelea na maboresho mbalimbali katika kuimarisha weledi na ubora wa Mawakili wa Serikali hivyo msituchoke pindi tutakapowahitaji katika hatua mbalimbali.

Kwa upekee kabisa napenda kumshukuru Mhe. Jaji Prof. John Ubena kwa kukubali kushiriki katika kazi hii pamoja na ratiba ngumu uliyonayo katika kutekeleza shughuli za Mahakama. Aidha, nimetaarifiwa kuwa umekubali kuwa Mhariri Mkuu wa Jarida la Uandishi wa Sheria Tanzania. Sina shaka weledi na uzoefu wako katika masuala ya kutafsiri sheria utakuwa na mchango mkubwa katika kukuza tasnia ya uandishi wa sheria Nchini.

Karibuni sana na nawatakia utekelezaji bora wa kazi hii.

Asanteni.

Hamza S. Johari
**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI**